

Mauaji ya karibuni Msumbiji

CHAMA cha wananchi wa Msumbiji, Frelimo kimetoa taarifa mjini Dar es Salaam jana kwa-mba maafa mengi yanatoka huko Msumbiji, na wananchi watatu wameweza kuuawa na kupigwa matako ya bunduki na Mreno.

Katika taarifa hiyo ni bure kabisa na ambayo imetiwa sahihi na Bwuna J. B. Chiteji, ofisa wa Frelimo inasema kuwa, mnamo tarehe 7.8.63 ofisa mmoja wa Kireno katika boma la Mueda alituma askari watatu kwenda kumkamata mwananchi mmoja katika kijiji Kunuma ambaye alisadikiwa kuwa ni mwanachama wa chama cha Frelimo, na mtu huyo alitiwa nguvuni na kufikishwa mikononi mwa Wareno ambao walitoa amri mtu huyo kupigwa na tako la banduki, ambaye ha-kuweza kuvumilia ali-kufa.

Alipigwa

Mwanachama mwingine ni Lukas ambaye pia alitiwa nguvuni siku ya tarehe 12/8/63 kwenye kijiji cha Mwidumbi na ye kadhalika alipigwa sana na Wareno hao mpaka akapata maafa, kifo cha aina hiyo pia kilitokea lea kwenye kijiji hicho hicho tarehe 15.8.63. Mwanamke mmoja aitwaye Thereza Munda ambaye pia alikuwa ni mwanachama wa chama cha Frelimo alikamatwa na kuchapwa sawa sawa mpaka akafa pale pale.

Silaha ya umoja

Taarifa hiyo ikamaliza kusema kuwa, Mreno anajitahidi kwa kila njia ili afanikiwe na ubeberu wake lakini ubeberu huo

bao ni wa maana kubwana hiyo hasa ndiyo kazi ya kujenga nchi. Akamaliza kuwa nchi hiwezi kujengeka kwa maneno tu bila ya vitemdo hivyo wananchi hao wameone!ena kuonyesha vitendo.

Silaha ya wanamsumbiji ni umoja kamili bila kujali ukabila audini bali kutaka ka kumuondo Mreno katika nchi ambayo ni rasli mali yao awaliyope wa na Mwenyezi Mungu, kwani, hawataki kutawala Ufaransa, Amerika, Italy, Poetugal, wala India bali wata-taka nchi yao ya Msumbji na Serkali ya watu weusi, wa Msumbiji ili maliza taarifa hiyo.